**KUTAFAKARI**:

Hakukuwa kilichobaki bila kusemwa. Yesu alikuwa haendi kubishana nao. Alikuwa amesema ukweli kuhusu ambayo yangetokea. Jitazame mwenyewe ukiwa umekaa karibu na meza pamoja na Yesu na marafiki hawa wote. Labda mmoja angesikia mwanguko hata wa kipini. Ukweli uliwanyamazisha. Walikaa hapo pasipokuamini lakini pia walimfahamu Yesu vizuri kiasi kwamba alikuwa hafanyi utani. Alikuwa hawafanyii mzaha.

- Unafiiri waliacha chumba wakitakari mioyoni mwao jinsi ya kumkosoa?
- Unafikiri Petro alikuwa akinug'unika moyoni akisema maneno kama, "Mimi, *sutaweza kufanya hivyo*"?
- Ukiacha chumba, unadhani ungekuwa unafikiri nini?

## MATUMIZI:

1. Wot tumesema, "Siwezi kufanya hivyo." Kumbuka wakati uliposema, "Nisingeweza

_____

_____

2. Ni jambo gani lilikuanya useme hivyo, "Sitaweza …?"

_____

_____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

3. Wengine walikusikia? Nao pia walikubali wasingeweza? Kulikuwa na hali gani kwenye chumba?

   _____

   _____

4. Umeshangaa kama ungemkana Yesu? Ni jambo gani lingekufanya umkane?

   _____

   _____

## **SALA**:

Ee Bwana, Unajua kama Petro ningesema, "Nisingeweza kufanya hivyo!" Na unajua kuwa nimefanya. Ninajuta moyoni mwangu. Na majuto haya yamenikamata. Yamenifanya nisiishi maisha ninayofahamu ungetaka niishi. Bwana Yesu, kuwa na neema na unihurumie. Nisamehe. Asante kwa kunirejesha katika uhusiano na Wewe ambao unaniweka huru kukutumikia kwa moyo wote. Asante kwa kunipenda na kunikaribisha katika uhusiano wa upendo pamoja na wewe. Na Bwana, Ulivyonisamehe, nifanye kuwasamehe wale waliosema, "Nisingeweza kufanya hivyo." Nipe moyo wa upendo na huruma ambao ambao unawaweka huru ili kuishi maisha huru na yaliyosamehewa.

_____

_____

_____

_____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

## SOMO LA TANO ~ Sehemu 1

### UTANGULIZI:

Petro amejifunza kuwa angefanya jambo ambalo halikutegemewa. Angemkana Yesu, rafiki yake, mwalimu wake, Bwana wake. Petro pamoja na hayo Petro alikataa kwa nguvu kukubli ambayo Yesu alisema kuhusu yeye. Kwa maneno Petro bado ana sema—"Sitaweza kukukana"—watu walianza kuondoka chumbani. Kutoka katika Injili inaonekana kama Yesu anatabiri kuhusu Petro lilikuwa ni jambo la mwisho alilowashirikisha. Mtu anaweza kukisia kilichokuwa kikiendelea katika mawazo ya wanafunzi. Walijua kuwa mmoja wao angemsaliti Bwana wao na Mkubwa wao na sasa wameambiwa kuwa Petro Mwamba angemkana wala si mara moja bali mara tatu. Wakiwa pamoja na Yesu waliondoka chumbani na kwenda nje usiku.

### KAZI YA KUFANYA:

Soma Mathayo 26:36-46. Kwas somo letu kimsingi tutatumia maelezo ya Mathayo kuhusu Yesu katika Bustani ya Gethsemane na kutumia Marko, Luka, na Yohana kwa taarifa za ziada.

- Yesu alikuwa akifanya nini bustanini?
- Waafunzi walikuwa wakifanya nini?
- Yesu alikuwa na wasiwasi gani kwa wanafunzi wake?

### ZOEZI:

1. Yesu alikwenda wapi pamoja na wanafunzi wake (mstari 36a)?

   _____

   Bustani hii ilikuwa wapi (Yohana 18:1; Luka 22:39)?

   _____

   _____

   Kumbuka: Huu ungekuwa muda mzuri kuwa na utaratibu wa kujizoesha ramani. Kwa historia chumba ambacho alikula karamu ya mwisho kilikuwa kusini magharibi mwa mji wa Asene. Baada ya chakula cha jioni, kama kawadia Yesu alikwenda na wanafunzi wake katika mlima wa Mizeituni kaskasini mashariki mwa mji. Walipaswa kuvuka bonde la Kidron ambalo linaelekea mashariki mwa Yerusalemu nje ya ukuta wa mji. Kushuka kutoka Yerusalemu kuna kilele cha Mlima Sayuni kwenda bondeni wangepanda tena kufanya njia yao kwenda Mlima Gethsemane katikati ya bustani kwenye miti ya mizeituni.
2. Yesu aliwaambia nini wanafunzi wake (mstari 36b)?

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

_____

3. Yesu aliwachukua aki na nani alipokwenda zaidi bustanini (Marko 14:33)?

_____

_____

4. Mathayo na Marko wanatumia maneno gani kuelezea hisia za Yesu?
   a. Mathayo 26:37, 38a _____
   b. Marko 14:33, 34

   _____

5. Maelekezo ya Yesu ni yapi kwa wanafunzi watatu aliokewnda nao (mstari 38b)?

   _____

   Katika Luka 22:40 Yesu yuko wazi zaidi. Anawaambia waombe kwaajili ya nini?

   _____

   _____

6. Yesu anawaacha na kwenda peke yake kuomba. Anamwomba nini Baba katika Mathayo 26:39?
   a. _____
   b. _____

7. Luka anaelezeaje kilichomtokea Yesu wakati akiomba (Luka 22:43-44)?

   _____

   _____

8. Baada ya Yesu kuomba aliwarudia wanafunzi wake. Alikuta nini kufuatana na Mathayo 26:40a?

   _____

9. Anamuuliza nini Petro (mstari 40b)?

   _____

10. Kwani nin ilikuwa ni muhimju kwa Yesu kwamba Petro akeshe na uomba (mstari 41)?

    _____

    _____

    Yesu alisema: " _____ ni radhi _____, bali _____ ni_____."

11. Yesu anafanya nini kufuatana na mstari wa 42?

    _____

    Saka yake ni ipi kwa wakati huu?

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

_____

_____

12. Yesu alikuta nini kwa mara ya pili lipokuja kwa wanafunzi (mstari 43)?

_____

_____

13. Aliwaacha tena_____

_____(mstari 44).

14. Yesu alipokuja mara hii (mstari wa 45-46)…

    a. Anauliza nini ? _____

    b. Anatamka nini ? _____

    c. Uamzi wake ni nini? _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

**Sehemu 2**

**FUNDISHO**: Yesu anaanza mateso yake kwa *mahangaiko* na *majonzi*. "Moyo wangu *umejawa na huzuni* kiasi cha kufa." Maneno haya yanaweza kupoteza maana yao ya tafasir; lakini pamoja na hayo wanaonyesha majonzi na masiktiko. Moyo wa Yesu ukotayari kupasuka kwa majonzi. Luka anasema, "Jasho lake yalikuwa kama matone ya damu yakidondoka ardhini." Tunapata majonzi ya Yesu tunaposikia sala yake: "…kama ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke (Mathayo 26:39)." Kikombe hiki kilikuwa ni nini? Isaya 51:17 anaongea juu ya "_____ _____." Yesu alikuwa karibu kupokea hasira kamili ya Mungu kwa kumfanya ababe dhambi za ulimwengu wote.

Kama Kristo alikuja duniani kuokoa wenye dhambi kutoka kwenye hasira ya Mungu, kwanini aliomba Baba kumuondlolea kikombe? Tunapaswa kufahamu kuwa Yesu alikuwa Mwana wa Mungu (umbo la ki-mungu) lakini pia mwana wa mtu (umbo la kibinadamu). Hakuna mwanadamu anayeweza kubeba hasira yote ya Mungu ambayo iliwekwa juu ya Mwana wake. Yesu alikuwa amefunikwa na majonzi. Yeye alikuwa tayari kubeba hasira ya Mungu kwaajili ya dhambi za wanadamu wote. Alikuwa aachwe na kutengwa na Mungu. Japo alikuwa amejaribiwa kukataa kikombe cha mateso akijua ugumu wake, Alikubali kwa unyenyekevu mapenzi ya Baba yake kwa kuomba.
"mapenzi yako yatimizwe." Yesu anasema katika Yohana 6:38, "_____ _____ _____ _____ _____." Yesu hakusita kutimiza mapenzi ya Baba. Badala yake ni kama Yesu alitazama kwenye saa yake na kusema, "Wakati umekaribia! Twende!"

**UTANGULIZI**: Mara tu baada ya Yesu kumaliza muda wake wa maombi alirudi kwa wanafunzi wake wengine waliokuwa wakisubiriJust. Kisha msaliti wake aliwasiri. Yesu alijua kuw awakati umetimia kwa Mwana wa Adamu kusalitiwa na kuwekwa mikononi mwa wenyedambi (Mathayo 26:45). Matendo yanaanza. Tumia hisia zako na na ujiweke kweye bustani wakati watu wanakuja kumkamata Yesu.

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Mathayo 26:47-56. Rejea anyingine zitahyusha Marko 14:43-50, Luka 22:57-54a, na Yohana 18:2-12.

**ZOEZI**: Hebu tuanze na Mathayo 26.

1. Ni nani anayejitokeza (mstari 47)? _____ kumbuka: Yohana anatwambia kuwa Yuda alijua mahali ambako Yesu angekuwa kwasababu Yesu alikuw akienda huko mara nyingi na wanafunzi wake (Yohana 18:2).
2. Amekuja na nani? _____
3. Wamejizatiti kwa _____ na _____. Wamebeba nini kufuatana na Yohana 18:3c? _____
4. Ni nani waliowatuma? _____
5. Alama ya msaliti ilikuwa ni nini (mstari 48)? _____
6. Yohana anaongeza. Yesu anaonekana kuchukua hatua. Ni swali gani alilowauliza wanaume (Yohana 18:4)? _____
7. Jibu lao lilikuwa ni nini (mstari 5a)? _____
8. Yesu liwaambia nini (mstari 5b)? _____
9. Kulitokea nini Yesu alipowaambia kuwa Yeye ni nani (mstari 6)? _____ _____
10. Katika mstari 7 na 8a mabadiliko yalirudiwa.
    a. Yesu alisema nini ? _____
    b. Majibu yao yalikuwa ni yapi? _____
11. Yesu alikuwa na hamu ya kutimiza mapenzi ya Baba. Yesu aliseme nini katika Yohana 6:39 Yohana anarudia tena katika Yohana 18:9b? _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

12. Kufuatana na 26:50 watu waliokuja na Yuda walisongea mbele wakamkata Yesu. Kulitokea nini baadae (mstari 51)? _____

_____

kumbuka: Tunaambiwa katiak Luka na Yohana kuwa mfuasi wa Yesu alikuwa Simoni Petro.

13. Amri ya Yesu alikuwa ni ipi (mstari 52a)?

_____

Yesu alimwambia nini Petro (mstari 52b)?

_____

_____

Yesu anajiweka chini ya mamlaka ya dunia. "

_____(verse 54)?"

14. Sasa Yesu anawahutubia makutano. Aliwauliza nini? _____

_____

kila siku alikuw hekaruni akifundisha. Hawakumkamata huko. Yesu alitaka kuweka wazi nini katika mstariw wa 56a? _____

_____

Kwa mara nyingine Yesu alitaka kuwaambia kuwa alikuwa chini ya mamlaka ya ulimwengu, maadiko ya manabii, kwamba lazima yatimizwe.

15. Yesu alikamatwa. Wanafunzi wote walifanya nini (mstari 56b)?

_____

**Sehemu ya 3**

**KUTAFAKARI**:

- Umati wa wanaume walimfuata Yuda na walikuja bustanini kumkamata Yesu. Maaskari na maofisa walikuja. Walitumwa na wakuu wa makuhani ana wazee wa watu. Walikuja wamejizatiti kwa silaa kama mapanga na miundu. Walikuwaja na mienge na taa. Walikuja na mamlaka na bado Yesu aliposema kuwa alikuwa ndiye Yesu wa Nazareti
- "walirejea nyuma na kuanguka chini." Hawa watu walikuja na mamlaka ya waliowatuma, walikuwa ni wanaume. Yesu alikuwapo kati yao kama mmoja aliye chini ya sheria ya maandkiko kutimiza mapenzi hay Baba.

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

- Kama unavyofikiri kuwa ungekuwamo kwenye habari hii, unajikuta umesimama wapi?
    - Pamoja na Yuda, soma kumsaliti kwa busu…
    - Pamoja na maaskari, soma kumkamata…
    - Pamoja na Petro, soma kumpigania…
    - Pamoja na wanafunzi wa Yesu, kutoroka na kukimbia…
- Ukao sawasawa na chaguo lako? Unaweza kuwa na sababu gani ya kuchagua kuwa ulikochagua? _____

**KUCHIMBA KWA KINA**: unahimizwa kusoma ambacho Isaya, mmoja wa manabii alichoandika kuhusu Yesu, Mashihi. Soma Isaya 53:1-12. Kupitia kumbukumbu ya ya somo hii la *Upendo wa Mungu Misia yetu* unahimizwa kurejea nyuma kwenye sura hii na kugundua jinsi Yesu anavyojionyesha kama mmoja aliye chini ya sheria ya maadiko. Tazama alivyochagua kuw amtii kwa mapnzi ya Baba ili kutimiza yale yote ambayo manabii waliandika kuhusu Yeye. Yesu ni Masihi, Waebrania ni Mpakwa mafuta (Isaya 61:1; Luke 4:18). Yesu ni Kristo, Kiyunani mpakwa mafuta!

**MATUMIZI**: Umati ulitumwa chini ya sheria ya maofisa na wazee. Yesu alitumwa na Baba na kujiweka chini ya mamlaka ya Maandiko. Ni nani aliyenituma?

- Ni chini ya mamlaka ya nani ninatafuta akuishi nikifanya mapenzi ya Baba wa ambinguni?

  _____

- Inaleta tofauti gani kuishi chini ya mamlaka haya jinsi ninavyoishi maisha yangu?

  _____

  _____

  _____

**KAZI YA KUFANYA**: Majaribu ya Yesu yalikuwa ni dhaaka. Kutoka Gethsemane alifungwa na kupelekwa kwa viongozi wa dini, maofisa wa mji, na liwali wa Waroma. Wakuu wa makuhani na Mafarisayo walikuwa wamepatana kumuua Yesu. Wasingevumilia tena mtu huyu aliyedai kuwa Masihi aliyeahidiwa ambeye Israeli walikuwa wakimsubiri kwa karne nyingi. Kituo cha kwanza cha njia ya kwenda msalabani kimeandikwa katika Injili ya Yohana. Soma Yohana 18:12-13, 19-24.

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

**ZOEZI**:

1. Maaskari na maofisa wa Kiyahudi walimpeleka wapi kwanza Yesu (mstari 13) _____
2. Tunaambiwa nini kuhusu Anasi katika mstari huu? _____
3. Tunaambiwa nini kuhusu Kayafa? _____
   Kayafa alitaniri nini katika Yohana 11:49-52 hii inarejea katika Yohana 18:14? _____
   _____
4. Sasa ruka chini hadi Yohana 18:19ff. Yesu ualiulizwa na Anasi, kuhani mkuu. Alimuuliza Yesu kuhusu nini (mstari 19)?
   a. _____
   b. _____
5. Kwa ufupi, Yesu alijibuje (matari wa 20-21)? _____
   _____
6. Mmoja wa maofisa alisemaje (mstari 22)? _____
   _____
7. Yesu aliitikiaje (mastari 23)? _____
   _____
8. Tambua kuwa hakuna kilichokamilishwa kwa maswali yao, Anasa alimtuma kwa nani (mstari 24)? _____

**Sehemu 4**

**ASSIGNMENT**: Soma Mathayo 26:57-68. Rejea nyingine zitakuwa ni Marko 14:53-65 na Luka 22:63-71. Japokuwa mpangilio unaweza ukavurugika, uliweke katika mawazo kuwa jaribu hili linafanyika usiku wa manane. Luka anatwambia kuwa ilikuwa _____ walipofika. Pia kumbuka kuwa kadiri masaa yalivyoendelea ndivyoYesu alivyovumilia mateso mikononi mwa maaskari na walinzi wakatili.

**ZOEZI**:

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

1. Yesu anapelekwa wapi (Mathayo 26:57)?

   _____

2. Ni aki na nani wote waliokusanyika?

   _____

   Kumbuka: Tunaambiwa kuwa Petro alikuwa akifuatilia kwa umbali wa usalama. Tutajifunza zaidi kuhusu Petro baadae katika somo hili.

3. Wakuu wa makuhani na na wakuu wa baraza walikuwa wakitafuta nini (matari wa 59)?

   _____

   _____ ili waweze _____.

   Kumbuka: The Sanhedrini ilikuwa ni kiako kilichokuwa na wakuu wa Makuani, waalimu, na wazee. Kimsingi walitawala Uyahudi lakini walipaswa kuishi kwa kutii sheria ya mamlaka ya Roma.

4. Waligundua nini (mstari 60)? _____

5. Mashahidi wa uongo walisema nini (mstari 61)? _____

   _____

   Inaposomwa katika hali halisi ukweli ulikuwa nini (Yohana 2:19-21)?

   _____

   _____

6. Kuhani mkuu alitaka Yesu aitikie mashtaka (mstari 62). Yesu alisema nini (mstari 63)?

   _____

   Rudi kwa Isaya 53. Kwa mujibu wa mazingira haya ambako Yesu alisimama mbele ya baraza na alishitakiwa kwa uongo, Isaya alielezeaje katiak mastari 7?

   _____

7. Kuahani Mkuu alitaka kujjua nini kutoka kwa Yesu katika Mathayo 26:63?

   _____

   _____

   Ukweli ni kwamba kuhani mkuu alitaka Yesu aseme kama Alikuwa Kristo au hapana, Masihi. Kama angesema kuwa ndiye Krsito basi angekuwa hatiani kwa kukufuru, kudai kuwa Mungu, jambo ambalo lngempasa ku _____ (mstari 66).

8. Jibu la Yesu ni lipi (mstari 64)? _____ Lakini anaendelea kusame, mwana wa Adamu, angeona_____."

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

Kayafa alikuwa amesikia ya kutosha. Yeye na maofisa wengine waliisha amua kinyume na Yesu. Waliamini kuwa maneno yake yalikuwa ya kufuru, sio ukweli. Kayafa alionyeshaje chuki yake juu ya majibu ya Yesu (mstari wa 65)? _____

9. Wote walimuhukumu Yesu kuwa anastahili kifo. Ni mambo gani yha kikatili waliyomfanyia (mstari 67-68)? _____
   Marko na Luka wanaelezea juu ya ukatili wa maaskari.

**KUTAFAKARI**:

- Unaweza kusikia Kayafa akimlaumu Yesu "chin ya kiapo cha Mungu aliye hai" kuanbia waliopo kama ni Kristo mwana wa Mungu? Labda unamuuliza Yesu swali kama lile. Itikio lako kwa jibu la Yesu ni nini? _____
  _____
- Je unaamini kuwa Yesu anasema kweli anaposema na mimi na wewwe, "Mimi ni Kristo Mwana wa Mungu aliye hai?" _____ inalta tofauti gani katika maisha yako ikiwa unaamini au hauamini kuwa Yeye ndiye.? _____
  _____

**KUCHIMBA KWA KINA**: Wakati wa utafiti huu Petro alikuwa amekaa nje Behewani. Huyu Petro aliandika kitabu cha 1 Petro kilichokaribu ya mwisho mwa Biblia. Fungua 1Petro 1 Peter 2:20b-23a. Petro aliwaandikia wakristo wapya waliokuwa sehemu ya kanisa la kwanza na anatuandikia wewe na mimi.

- Ansema "_____." Mstari wa 22 ni nukuu ya kutoka nabii Isaya. (Isaya 53:9) "_____."

**MASWALI YA MATUMIZI**: Kristo alivumilia mateso japo hakutenda baya lolote. Ameniachia mfano na ameniita kumfuata kwenye nyao zake. Kuitwa kufuata nyayo zake zinaleta aleta mabadiliko gani katika utaratibu wangu wa maisha? Wito wake unaleta tofauti? _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

_____

_____

**Sehemu 5**

**ZOEZI**: Kabla ya kuendelea na kujaribiwa kwa Yesu tunapaswa kujifunza kilichokuwa kikiendelea kwenye behewa kwa kuhani mkuu.

1. Mathayo 26:58, Marko 14:54, na Luka 22:54 wanatwambia nini kuhusu Luka?_____

   _____

2. Yohana 18:15 na 16 inatupa sehemu ya habari. Yohana anatwambia nini?
   a. Huyu mwanafunzi mwingine alikuwa ni nani? _____
   b. Yohana alimfahamu nini? _____
   c. Hii ilimpa nafasi katika behewa la kuhani mkuu ambako Anasi na maofisa wengine, mafarisayo, na wakuu wa makuhani walikuwa wamekusanyika. Lakini, vipi kuhusu Petro? Petro alikuwa amesubiri wapi?_____
   d. Petro aliingiaje kwenye behewa (mastari 16)? _____

      _____

3. Petro sasa yuko behewani na wengine. Yohana 18:18 anatupa picha: "…_____." Tumepata picha.
4. Binti aliyekuwa kwenyezamu, labda aliyemruhudu Petro kuingia alimuuliza nini ( Yohana 18:17a)? _____
   a. Petro alijibu (mstari 17b)? "_____."
   b. Luka 22:55 anatwmbia kuwa Petro alikuwa ameketi chini karibu na moto na kwasaidiwa na mwanga akamkazia macho na kusema mwanga wa moto (mstari 56), "_____

      _____."
   c. Na Petro akajibu, "_____."

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

d. Katika Mathayo 26:70 inaposemwa kuwa alikuwa na Yesu wa Galilaya, Petro alikana mbele ya watu wote. "_____."

e. Marko 14:68 inaema kuwa Petro alikana kuwa alikuw ana Mnazareti, Yesu.. "_____

_____" na akatoka nje.

5. Yesu alikuwa ametabiri kuwa angemkana mara tatu. Tunaambiwa nini kuhusu mara nyingine mbili katika Rejea zinazofuata?

a. Mathayo 26:71-74a - _____

_____

b. Marko 14:69-71 -

_____

_____

c. Luka 22:58-60 - _____

_____

d. Yohana 18:25-27a) -

_____

_____

6. Jogoo aliwika. Unabii wa Yesu ulitimia kwa Petro. Alikumbuka maneno Yesu aliyosema (Mathayo 26:75a): "_____

_____."

7. Na Petro (mstari 75b)… _____

8. Luka anaogeza kitu kwa wakati huo. Luka 22:61 anatwambia kuwa _____

_____.

**MASWALI YA KUFIKIRIA**: Yesu alikuwa akiwasiliana kwa kukemea au kwa huruma? Mstari 61unasema, "Kisha Petro _____ …" Hii inaweza kutwwambia nini kuhusu kutazama kwa Yesu? _____

_____

Tazama pia 2 Wakorintho 7:10. Mawazo na tafakari yako: _____

_____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

**Sehemu ya 6**

**KUTAFAKARI**:

- Inamsumbuaje Petro. Masaa tu baada ya kusema kwa mkazo kuwa *asingeweza*… na ni muda mfupi tu anafanya kile alichosema kuwa asingefanya. AlimkanaYesu, Bwaa wake, ambaye alimkiri kuwa_____ (Mathayo 16:16). Na hakumkana mara moja bali mara tatu!
- Tunaambiwa kuwa Yesu aligeuka akamtazama moja kwa moja Petro. Petro alikumbuka maneno aliyokuwa amemwambia. Kwa kuangalia macho ya Yesu ilimweka Petro katika majonzi makubwa na kujutia alilolifanya. Alimkana ambaye asingemkana bali angesurubiwa kwa hiari kwaajili yake. alikwenda nje akalia kwa uchungu.
- Usiku peke yake alikabiliana na ukweli wa tabia yake ya dhambi. Ilikuwa zaida alichofanya kilichomfanya Petro awe na uchungu. Maneno yake ya kukana yalikuwa yanadhihirisha hali ya moyo wake. Pia yeye alichukuliwa mimba katika dhambi. Zaidi ya upendo wa aliyekuwa akienda msalabani Petro alijua kuwa hana wokovu. Pasipo na mashaka Petro alikumbuka maneno aliyoambiwa na Yesu. (Mathayo 26:41) Alipokuta wanafunzi wamelala: "_____ _____." Kisha aliongeza, "_____ _____."

  Bwana alijua nia ya Petro ya kutenda mema lakini pia alijua nguvu ya majaribu. Yesu pia alikuwa amemwambia Petro kuwa amemuombea kuwa imani yake sitindeke. Ni nguvu kiasi gani aliyopewa Petro usiku huo wa masiktiko na aibu kwasababu alijua kuwa Yesu alikuwa amemuombea kuwa imani yake isitindike? _____

**MATUMIZI**:

1. Kumiliki maneno na matendo ya binafsi ni vigumu inapodai kukiri makosa yale ambayo mtu alidhani kuwa hayawezekani. Tangao la letu kama Petro, "Hata kama kila mmoja

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

ange _____, Nisinge!" Jaza nafasi wazi. "Hata kama kila mtu angebishana nawe, nisinge!" "Hata kila mtu angekuwa mbaya akimsema bosi, Nisingefanya hivyo!" hata kama kila mtu angefanya udanganyifu kwenye kodi, Nisinge!"

2. Ni mambo gani yanaendelea kwenye mawazo yako sasa?

   _____

   _____

3. Inaweza kuwa vigumu kukumbuka ambacho hauamini kuwa ungeweza kufanya.
   - Jikubali kitu ambacho emefanya. Kumbuka wakati.

     _____
   - Ni watu gani waliohusika? Ni maneno gani yaliyosemwa/hatua iliyochukuliwa?

     _____
   - Matokeo yalikuwa ni nini?

     _____
   - uliitiieje ulipofanya yale amboyo ulisema usingefanya?

     _____

**KUKARIRI**: Habari haishii kwa kutuachia jambo ambalo linatufanya iwe vigumu kusamehe nafsi zetu au jambo ambalo hatuamini kuwa Mungu hawezi kutusamehe. 2 Wakorintho 7:10 inatupatia kila mmoja wetu habari njema! "_____ _____ _____ _____." Hakikisha kuwa unaandika kifungu hiki kwenye kadi na ukiweke kwenye benki ya kumbukumbu yako. Toba huelekeza kwenye wokovu na afya nzuri! Majuto ya kimungu huwezesha Mungu kuzungumza neno la msamaha kwetu na vikwazo haviwezi tena kututenga na Mungu na wale tuliowakosea.

**SALA**: Bwana Yesu, ni vigumu kuamini kuwa ningekukana kama Petro alivyofanya. Ninaomba niamini kuwa nisingeweza kufanya hivyo. Lakini nikijiangalia kwa ukweli katika maisha yangu, ninaona kuwa nimekutenda dhambi, kwa mawazo, neno, na matendo. Ninajua kuwa nimekukana mbele ya wengine, hasa nilipotaka kukubalika na kuungwa mkono na wao. Nisamehe Bwana Yesu. Ninaweza tu kutubu na kuamini katika ahadi yako kuwa "majuto ya kimungu huelekeza kwenye wokovu." Ponya roho yangu ya kiu ambayo inangoja kunywa katika mambo ya dunia hii badala ya kunywa haki yako. Asante kwa kutazama kwako kwa upendo ambako hunisamehe

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

kutoka kwenye uchafu wote.

_____

_____

_____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

**SOMO LA 6**

**Sehemu ya 1**

**UTANGULIZI**: Katika somo la 3 tulijifunza kuhusu kukana kwa Petro na jinsi alivyolia kwa uchungu kwa ukweli kuwa alikuwa amemkana Bwana wake. Lakini kulitokea nini kwa Yuda, aliyemsaliti? Mara ya mwisho tulisikia habari zake alipomsaliti Yesu katika Bustani ya Gethsemane ambako Yesu alikuwa akiomba. Ni Mathayo tu anaandika juu ya yaliyompata Yuda.

KAZI YA KUFANYA

Soma Mathayo 27:1-10

- Yuda alikubali nini?
- Wenzake walijibu nini?
- Yuda alichukua hatua gani?

**ZOEZI**:

1. Tunaambiwa kuwa uamzi wa makuhani wakuu na wazee ulikuwa ni nini (mstari 1)? _____

   _____

2. Kwahiyo wanasema _____ _____ (mstari 2).
3. Ni nini kinaonekana kumshangaza Yuda, msaliti (mstari 3a)? _____
4. Alikamatwa na _____ vipande vya _____ (mstari 3b). alivirudisha kwa nani? _____

   _____

5. Yuda aliwaambia nini (mstari wa 4a)? _____
6. Kwa vyovyote, wakuu wa makuhani na wazee wasingechukua wajibu wa usaliti wa Yuda kwa Yesu. Walijibu nini? _____
7. Yuda alifanya nini (mstari 5)?
   a. _____
   b. _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

c. _____

8. Wakuu wa mauhani waliachwa na pesa na ilibidi waamue cha kuzifanyia. Kwanini pesa haikuwezekana kuwekwa kwenye hazina (mstari 6)? _____
9. Waliamua pesa kuzifanyia nini (mastari7)? _____
10. Eneo la mazishi linaitwaje (mstari 8)? _____
11. Unabii mwingine ulitimizwa katika Mathayo 27:9-10. Yeremia alisemaje? _____

_____

**KUTAFAKARI**:

- Yuda alikuwa mtu aliyefuata *a*liyoyaamini kuwa ni kweli kuhusu Yesu. Aliamini kuwa Yesu ni Masihi, Aliyeahidiwa, lakini aliamini kama Wayahudi walio wengi kuwa Masihi angekuja na kutawala kama mfalme wa kisiasa mwenye nguvu za kupindua serikali ya kikatili ya Waroma. Kama Yesu angeanzisha ufalme wa kidunia, Yuda alikuwa na matumaini makubwa ya kupata nafasi kubwa katika ufalme. Pamoja na hayo Yesu aliongelea juu ya ufalme tofauti, si wa dunia hii.
- Tunapata picha nyingine ya Yuda katika Yohana 12:4-6. Kwa vyovyote Yuda alikuwa ameonyesha ujuzi fulani ndiyo maana aliteuliwa kuwa mtunza pesa wa wanafunzi. Mistari hii inaonyesha nini kuhusu moyo wa Yuda na tabia yake? _____

  _____
- Ni picha ya kusikitisha. Yuda alimsaliti Yesu na kutundikwa, na kupigiliwa misumari msalabani. Kifo cha Yuda kilikuwa cha kujiua. Alijitundika kwa mti wake mwenyewe, mti ambao haukutoa msamaha. Maisha yake kama mwizi na mnafiki, mwongo na msaliti, alikuwa hajajazwa na matumaini ya uzima wa milele, bali alikuwa anakimbilia ndoto zote na matumaini ya maisha ambayo yangemfanya mkubwa mbele za wengine. Bila matumaini, bila toba, na bila msamaha alifariki akiwa amehukumiwa kwa hukumi ya milele.
- Fikiria tofauti kati ya Petro na Yuda. Kila mtu aliamini nini kuhusu Yesu kwamba alikuwa nani na kwa nini alikuja?

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

| **Rejea** | **Petro** |
|---|---|
| Mathayo 16:15-16 | |
| Yohana 6:68 | |
| Yohana 6:69 | |

| **Rejea** | **Yuda** |
|---|---|
| Yohana 6:63b-64 | |
| Yohana 6:70-71 | |
| Yohana 8:44-47 | |
| Yohana 12:6 | |

**KUTAFAKARI**: Chukua muda tena kurudia 2 Wakorintho 7:10. Neno hili linatuambia nini kuhusu rejea kati ya Petro na Yuda? Linatuelezea nini kuhusu uhusiano kila mmoja aliokuwa nao na Yesu? _____

_____

_____

**SALA**: Bwana, kama Petro ninatangaza, "Una Neno la uzima wa milele." Roho Mtakatifu amenipa imani kuamini na kujua kuwa Wewe, Yesu, ni Mtakatifu wa Mungu. Kama Petro, ninaishi kwa matumaini na kutamka, "Wewe ni Kristo Mwana wa Mungu aliye hai." Kama Petro hii imefunuliwa kwangu na Baba wa mbinguni. Maneno haya yananipa faraja kubwa sana! Ninajua kuwa pamoja na yote ninayoyafanya na kusema, pamoja na mawazo maovu na makusudi, haijalishi, ninachojua ni kwamba ninaishi nikiwa ninapendwa na kusamehewa. Kwako peke yako ninakupa shukrani zangu na sifa._____

_____

_____

_____

**Sehemu 2**

**UTANGULIZI**: Yesu alimaliza mahojiano yake mbele ya Anasi mmoja wa wajumbe wa baraza. Alipigwa vibao, alidhihakiwa, alifungwa kitambaa machoni, alitemewa mate, na

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

kupigwa. Waliokuwapo walimshuhudia uongo juu yake. alishitakiwa kwa kukufuru na kisha akahukumiwa kifo. Asubuhi na mapema mbele ya kila mtu, wakiwapo wajumbe wa baraza, maamuzi yalifanyika (Marko 15:1). Walimfunga Yesu, walimpeleka wakamkabidhi kwa Pilato (Luka 23:1). Kuna uwezekano kuwa ni katika safari haii Yesu alimtazama Petro aliyemkana.

Uliweke maanani unaposoma kuwa Yesu alifanyiwa haya usiku mzima, mwishoni mwa juma alipata suruba za wote walikusanyaika wakimdhiaki kwa mfururizo. Alitembea kwa miguu kutoka chumba cha ghorofa kutoka kona ya kusini magharibi ya Yerusalemu ambako chakula cha Pasaka kilifanyika, kona ya kaskazinimagharibi nje ya mji kwenda Gethsemane. Maaskari waliomkamata walimrudisha nyuma kusini magharibi mwa mji kwenda nyumbani kwa Kayafa ambaye tena alimtuma kwenye ikulu ya Pilato.

Pointi moja zaidi kabla ya kuendelea. Kila moja ya Injii nne (Mathayo, Marko, Luka, na Yohana) inasema juu ya majaribu ya Yesu, kuteswa kwake, na kifo chake. Kmbuka kuwa kila mwandishi wa Injiili alikuwa akiandika kuwafikia wasomaji wake. Kwahiyo kila mmoja alikuwa na makusudi tofauti kwa kila kilichomo kwenye kitabu alichoandika. Tutaendelea na masomo yetu katika Injili ya Luka.

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Luka 23:1-7.

- Yesu alitumwa wapi baadae?
- Mashitaka yalikuwa ni yapi?
- Hitimisho la Pilato lilikuwa ni nini?

**ZOEZI**:

Mkutano unampeleka wapi Yesu (mstari 1)? _____

Pilato alikuwa liwaliwa Waroma katika Yudea wakati wa Yesu tangu 26 A.D. to 36 A.D. Hakuna mengi yanayofahamika kuhusu yeye bali tunafahamu kuwa kuteuliwa kwake kutawala Uyahudi hakukupendwa na wengi. Tunajua kuwa nafasi ya pilato kisiasa ingeingia matatani kama kungetokea mgomo kwenye utawala wake. Tukiwa na hali hiyo kwenye mawazo yetu hebu tuendelee …

1. Mashitaka mengi juu ya Yesu yalitolewa. Walidai nini (mstari wa 2)?
   a. _____
   b. _____
   c. _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

2. Pilato alimuuliza nini Yesu (mstari 3)?

   _____

   Na Yesu alijibu, "_____."

3. Pilato alitangaza nini kwa washitaki wa Yesu (mstari 4)? _____

   _____

4. Watu walisisitiza _____ _____ _____ (mstari 5). Nchi hii ilikuwa chini ya utawala wa Pilato.

5. Walidai nini kuhusu mafundisho ya Yesu? _____

   _____

6. Sasa, Pilato alitaka kufahamu nini (mstari 6)? _____

7. Pilato alitafuta njia ya kujiondoa katika matatizo. Yesu alikuwa chini ya mamlaka ya _____. Kwahiyo Pilato alifanya nini (mstari 7)?

   _____

   Tunajua kuwa kwanza Yesu alipelekwa kwa Anasi na kisha kwa Kayafa. Makutano pamoja na Kayafa waliamua kuwa Yesu anapaswa kufa kwasababu ya kukufuru, kwasababu ya aliyedai kuwa. Makuhani wakuu na maofisa wengine hawakuwa na mamlaka ya kumuhukumu kwahiyo walimkabidhi kwa Pilato. Luka ni mwandishi pekee anayesema kuwa baada ya Pilato kukuna kwa mara ya kwanza na Yesu alimtuma kwa Herode.

   Inawezekana Herode alikuja kutembelea Galilaya kwaajili ya sherehe za Pasaka. Ikulu yake haikuwa mbali na nyumba ya Kayafa Magharibi mwa Yerusalemu. Herode alichukua hatua gani kwa Yesu (mstari 8a)? _____

   a. Kwanini (mstari 8b)?

      _____

   b. Kwanini (mstari 8c)?

      _____

8. mstari 9: Herode

   _____

   Lakini Yesu

   _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

9. Mstari 10: Wakuu wa makuhani na waalimu _____
10. Mstari wa 11a: Herode na maaskari wake_____

    Mstari 11b: Walimrudisha kwa _____.
11. Tunajifunza nini kuhusu uhusiano wa Herode na Pilato mstari wa 12? _____ _____

**Sehemu 3**

**KUTAFAKARI**:

- Hakuna aliyeonekana kuwa anajua cha kumfanya Yesu. Waliotaka kumuua hawakuwa na mamlaka. Aliyekuwa na mamlaka alimkuta hana kosa la kuhukumiwa kifo. Mtu yoyote hawezi kusaidia bali kuuliza swali: nimemfanya nini Yesu? _____ _____

  Nikijiunga na wale wanaotaka kumuua, ningefanya hivyo kwasababu…
  - Kwasababu ya alivyojidai kuwa? _____ _____
  - Kwasababu ya mafundisho yake makali ya kuniita nitubu? _____ _____
  - Ni chukizao maishani mwangu kwa kuendelea kuniudhi? _____ _____

  Tena nimemfanya nini Yesu? _____
- Herode alifurahi kumuona Yesu. Alitaka kuona miujiza. Kutuatana na aliyosikia kuhudu Yesu, alitegemea kuona baadhi ya miujiza. Badali yake, Herode hukutaka kumpa Yesu hata nafasi ya kuongea. Kwa vyvyote asingemruhusu atende muujiza wowote. Na vipi kuhusu mimi? Je niko kama Herode? Je ninataka kuona Yesu atakavyonifanyia? Ninataka anitendee muujiza gani sasa? Ajira mpya? Gari la kifahari? uponyaji? Kupata

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

mimba? Ni muujiza gani ninataka atende kabla ya kumuamini? _____

_____

inngenigharimu nini kukubali kuwa ninasubiri kuona mazingaomwe ya nguvu za Mungu kabla ya kumuamini kwa imani kuwa Yesu ni Kristo, Mwokozi *wangu* na mkombozi *wangu*? _____

_____

- Washitaki wa Yesu walikuwa na jazba ya nguvu. Walikuwa makatili kwasababu walitaka auawe. Ninafananaje na washitaki wake? Je nimemkasirikia Yesu? Aliniangusha? Hakufanya nilichotegemea afanye? Kwanini ananifanya niwe mgonjwa wa akili? Kwanini sitaki kubadili mawazo yangu juu yake? Ni jambo gani lililonifunga na halitaki kuniachilia kuelewa upendo wake kwaajili yangu? _____

  _____

- Herode na maaskari wake walimkejeliYesu. Walimdhiaki na kumdhalilisha, walimfunika na joho la thamani, na kumtuma aliyekuwa akijiita Mfalme wa Wayahudi kwa Pilato tena. Je ninamkejeli Yesu? Je Yesu ni kitu changu cha kutania? Ni jambo gani linanifanya kumsema maneno ya utani Yesu, kumdhiaki na kumpuuza, kumvika na na kumfanya aonekane kama mjinga badala ya kumwabudu na kumuheshimu kama Mwana wa Mungu? _____

  _____

**SALA**: Chukua muda wa toba kukubli ilivyomfanyia Yesu. Kuja mbele za Mungu kwa uvumilivu na toba ukimshukuru kwa kuteswa kwaniaba yako japo ukiwa na Pilato unajua hitaji la kukubali kuwa "unatafuta sababu yoyote ya kumuhukumu huyu mtu." _____

_____

_____

Kisha, sikiliza kwa karibu Habari Njema ya Mungu kwaaji yako unapotafakari maneno haya, _____." (1 Yohana 1:9).

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

**Sehemu 4**

**UTANGULIZI**: Yesu alirudishwa kwa Pilato. Matatizo yalirudi mikononi mwa Pilato. Alikuwa anakwenda kufanya nini na mtu huyu anayeitwa Yesu? Tunajua mwingene alivyomfanyia Yesu. Sasa ni wakati wa Pilato kuonyesha tabia yake.

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Luka 23:13-25.

- Pilato alikusanya aki na nani?
- Umati ulisisitiza nani aachiliwe?
- Pilato alikuwa amfanyie nini Yesu?
- Uamzi wa Pilato ulikuwa nini?

**ZOEZI**:

1. Pilato aliwaita nani pamoja (mstari 13)?
   _____
2. Aliwaambia nini?
   a. Mstari 14a: _____
   b. Mstari 14b: _____
   c. Mstari 14c: _____
3. Pilato alisema nini kuhusu Herode (matari 15a)?
   _____
4. Pilato alisema nini kuhusu Yesu (matari 15b)?
   _____
5. Pilato aliwaambia watu kuwa anakwenda kufanya nin (mstari 16)?
   _____
   _____

   Kumbuka: Adhabu ya Waroma ilikuwa ya kikatili kiasi kwamba wafungwa wangekufa kabla ya hukumu yao. Adhabu ilihusisha kutandika viboko

   **FUNDISHO**: Ilikuwa ni utamadumi kuwa siku ya sikukuu ya Pasaka aliachiwa mfungwa mmoja aliyechaguliwa na watu (Mathayo 27:15ff). kufuatana na Mathayo 27:17 tunajifunza kuwa fursa ambayo Pilato alitoa kwa umati wa watu ililenga kuachaia

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

_____ au kuachia _____. Tunajifunza nini kuhusu Baraba katika Mathayo 27:16 na Luka 23:19?

_____

**ZOEZI**:

1. Umati wa watu ulikuwa umeshawishiwa na wakuu wa makuhani na wazee (Mathayo 27:20). Watu waliitikiaje walipoulizwa na Pilato kuwa kati ya wawili nani wangetaka aachiwe (mstari 21)? _____
2. Lakini Luka 23:20 inatwambia kuwa Pilato alitaka aachiwe Yesu. Kwahiyo alifanyaje? _____

   _____
3. Umati uliendelea kutoa kelele gani (mstari 21)?

   _____
4. Kuhusu hatua hii ya kujaribiwa Mathayo peke yake anatwambia kwa ufupi kilichotokea. Soma Mathayo 27:19. Kulitokea nini?

   _____

   Ujumbe unasemaje? _____

   _____
5. Kwa mara ya tatu Pilato anaongea na umati (mistari 4, 14, 22). Anawauliza nini (Luka 23:22)? _____

   alisena nini kuhusu Yesu?_____
6. Umati wa watu ulidai nini (mastari 23)? _____
7. Uamzi wa mwisho wa Pilato ulikuwa ni nini (mstari 23)?

   _____
8. Alimwachia _____, chaguo la watu (mstari 24, 25), na Yesu_____.
9. Tunajifunza nini kuhusu Pilato katika rejea hizi?
   a. Marko 15:15

      _____
   b. Yohana 19:12-13

      _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

c. Mathayo 27:24-26 _____

10. Tunaambiwa nini kuhusu Yesu alivyotedewa na maaskari wa mariwali katika Mathayo 27:27-31?
    a. Walimvishaje? _____
    b. Walimtukanaje? _____

    _____
11. Tena yanakuja maneno toka mstari wa 31: "Kisha _____." Nabii Isaya anaongea juu ya Yesu katika Isaya 53:7. Nabii anasema nini? " _____ _____."

**Sehemu 5**

**KUTAFAKARI**: Ingekuwa vizuri kutafakari juu ya habari ya mateso badala ya kutumia muda kutafakari kuhusu mfungwa aliyeachiwa sasa hivi kuoka kwemye hukumu kwa kosa la uani na mauaji. Mathayo anamsema Baraba kama mfungwa sugu.

Tunaweza kusikia umati wa watu wakipiga kelele mbele ya Pilato, "Msulibishe! Msulibishe!" Inaonekana kuwa, gereza ambalo Barnaba alikuwa amefjngwa lilikuwa karibu na Pratorio ambapo Baraba alisikia kelele za watu. Asingeweza kusikia swali Pilato alilouliza Pilato aliuliza, lakini fikiria kwa muda mfupi ambavyo ingekuwa. Alikuwa mfungwa wa uasi na mausi. Kifo kilikuwa ndiyo hukumu yake.

Pilato aliuliza swali: "kati ya wawili mnataka nimwachie yupi? Umati ulijibu, *"Baraba!"* swali la pili Pilato aliuliza: "Nimfanyeje Yesu anayeitwa Kristo?" Umatti ukapiga kelele, *"Msulibishe!"* Tena Pilato angeuliza, "Kwanini? Ametenda kosa gani?" wamgepiga kelele zaidi, *"Msulibishe!"*

Chukua muda ujitazame ukiwa kifungoni. Wewe ni Baraba. Sasa soma maneno katika italiki unayosikia. Badilishas jina *lako*, kama wewe ni mwanamke badili jina la kike liwe la kiume.

- Unafikiri nini? _____

  _____
- Ni jambo gani karibu litatokea kwako?

  _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

Unajua kuwa utaadhibiwa kwa kosa lako na unajua na unajua adhabu ni kifo!

Chukua muda na uendelee kutafakari. Fikiria Baraba alichofikiri wakati mkuu wa gereza alipokuja na kumwambia ameruhusiwa kutoka gerezani na kwamba Yesu angesurubiwa kwaajili yake. Inasikika kama haiaminiki? Yesu alikufa kwa niaba ya Baraba moja kwa moja. Yesu alikuwa sadaka ya dhambi zake na dhambi za ulimwengu.

Nabii Isaya anazungumzia Yesu jinsi alivyofanyika niaba yetu Isaya 53:4-5. Andika mistari nii na kujifunza jinsi Yesu alivyotoa maisha yake kwaniaba yako na yangu: _____

_____

_____

_____

Yesu alichukua uovu *wetu* na kubeba huzuni *yetu*. Alitobolewa kwaajili ya maovu yetu, Alichubuliwa kwaajili ya maovu *yetu* ; adhabu ya amani yetu ilikuwa *juu yake*, na kwa majeraha yake sisi tunapona.

Mara baada ya Baraba kuachiliwa hatujui alifanya nini. Aliyesulibiwa kwaniaba yake, akipigiliwa misumari? Alisema neno, "Anakufa kwaniaba yangu? Je alikuwa na taarifa kuwa Yesu hakufanya lolote baya au Alikuwa Mwana wa Mungu? Je hilo lingeleta tofauti fulani kwake? Kwa vyovyote, hatujui jibu kwa maswali haya lakini tunaweza kukisia jinsi jinsi ilivyokuwa kwa kurejewa uhai wake. Na alikwenda wapi usiku ule? Alimwambia nani kuhusu kuachiliwa kwake?

Sawa na jinsi Baraba alivyoachiliwa kutoka adhabu ya kifo kutokana na mambo yake yaliyopita. Tumewekwa huru. Sasa tuko huru kuishi maisha mapya yaliyojaa matumaini na mambo yajayo, maisha yajayo pamoja naye umilele! Kwaababu Yesu alibeba adhabu yetu tunasimama mbele ya Baba bila kitu isipokuwa Neno lake linalotwambia kuwa tumesamehewa! Sasa hakuna chochote katika viumbe kinachoweza kututenga na upendo wa Mungu ambao ni wetu katika Kristo Yesu Bwana wetu (Warumi 8:39).

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

**MASWALI YA MATUMIZI**: Mimi na wewe tumeachiliwa kutoka kifungoni kwasababu Yesu alikufa kwaniaba yetu. Nitakwenenda kufanya nini? Hii italeta tofauti gani katika maisha yetu kutokana na kuachiliwa? Ninakwendas kusherekea uhuru wangu? Je ninakwenda kusahau na kuishi kama siku zote nilivoishi zamani? Itikio la uhuru wangu utakuwaje? Nimenusurika kifo!

1. Ninataka kumjua aliyekufa kwaniaba yangu. Nitakwenda kumjua kwa njia ya…
    a. _____
    b. _____
    c. _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

**SOMO LA 7**

**Sehemu ya 1**

**UTANGULIZI**: Maisha yote ya Yesu watu walitaka kumuua. Katika Mathayo 2:2 Majajusi kutoka mashariki walikuja Yerusalemu wakiuliza, "Yuko wapi aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?" Huyu mfalme waliyekuwa wakimtafuta hakuwa mfalme wa dunia (Yohana 18:36) Lakini aliyekuja kama Kristo, aliyetabiriwa na manabii kuwa angekuja. Mfalme ambaye Wayahudu walikuwa wakisubiri, pamoja na hayo waliamini kuwa angekuwa mfalme ambaye angetawala Israeli na kuwaweka huru kutoka utawala wa Waroma. Kwahiyo Mamajusi walikuja Yerusalemu wakiwa na furaha kuabudu aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi. Lakini Mfalme Erode Mkuu alichukua hatu gani juu kuhusu habari hizo za Masihi, mfalme wa Wayahudi alizaliwa (Mathayo 2:8, 13b, 16)?

_____

In John 1:49 Nathaniel made a profound declaration. What did he say about Jesus? _____

_____

**KAZI YA KUFANYA**: Soma Yohana 18:33-19:16.

**ZOEZI**:

1. Yesu alikuwa kweli Mfalme wa Israeli! Sasa Pilato Riwali wa Kiroma, anamuliza Yesu kuwa Wayahudi walimshitaki kuwa ni mtu aliyekufuru, na alipaswa kupata adhabu ya kifo. Swali lilikuwa ni lipi (Yohana 18:33)?
   _____
2. Yesu aliseme nini kuhusu ufalme wake 36? _____
   _____
3. Pilato alitamka, "_____ (mstari wa 37)!"
   a. Yesu alimjibu, "_____."
   b. Yesu alimwambia Pilato kuwa alikuja kama mflame ili kushuhudia _____.

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

c. Katika mstari wa 38 Pilato anauliza ambalo watu bado wanauliza hata leo: _____

_____

4. Pilato alikwenda nje kwa Wayahudi na kusema, "_____

_____(mstari wa 38)."
5. Hata maaskari wa Pilato walimdhiaki Yesu kwa kumvika vazi la zambarau na kutengeneza taji la miimba na kusema, "_____ (Yohana 19:3)."
6. Kwa mara nyingine Pilato kwenda kwa Wayahudi (mstari wa 4) na kusema, "_____

_____
7. Wakuu wa makuhani na maafisa walipomuona Yesu akiwa katika vazi la zambarau na kuvaa taji ya miibawalipiga kelele, "_____! _____!"
8. Mstari 6b: Pilato aliendelea kusisitiza: "_____."
9. Lakini Wayahudi waligundua mchezo mbaya wa pilato. Walipiga kelele gani katika mstari wa 12? _____

_____
10. Pilato anamtoa Yesu nje. Anakaa kwenye kiti cha hukumu na kusema, _____ (mstari wa 14b)
11. Walipiga kelele, _____(mstari 15)
12. Pilato aliuliza,

_____
13. Kuhani mkuu alijibu, _____
14. Pilato alishindwa na kelele za watu na kuwakabidhi Yesu _____ (matari 16).

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

**Sehemu 2**

**KUTAFAKARI**:

- Kwanini watu walikusundia kumsulubisha Yesu wakati siku chache zilizopita walikuwa wakiimba, "Mbalikiwa ni Mfalme ajaye kwa jina la Bwana (Luka 19:38)!" Ni kitu gani kiliingilia na kuharibu? Ni kitu gani kilichobadilisha mawazo yao? Kwahiyo wameanza kugundua kuwa wamedanganywa kwamba madai yake ya kuwa mfalme wa Wayahudi yalikuwa ya uongo? Miujiza yake imewapofusha na kuwafanya wasihamu kuwa Yeye ni nani? Au wamekamatwa kwa muda mfupi, na jaziba ya umati wa watu…

  Au inawezekana huu ulikuwa ni umati wa watu tofauti… Mfalme mwingine alikuja Yerusalemu siku za kabla ya Pasaka. Herode Antipa, mtoto wa Herode Mkuu, alifika kutoka Galilaya alikokuwa akitawala kuja kusherekea Pasaka. Kwavyovyote aliingia na msafara wa maasari pamoja na farasi. Pilato pia alisafiri kuja Yerusalemu kutoka ikulu yake Kaisaria pamoja na maaskari, akilenga kutunza amani wakati wa Pasaka. Uwepo wake ulikuwa inahakikishia Wayahudi kuwa wanaishi chini ya mamlaka ya Roma.

  Kwahiyo ni nini kiliwafanya watu waliokuwapo kuanza kusema, "Msulibishe! msulibishe! Mawazo yako:

  _____

  _____

  _____

**MATUMIZI**:

- Kama ungekuwa kwenye umati, unafikiri ungepiga kelele gani? _____

  _____

- Kwanini?

  _____

  _____

**KUTAFAKARI**:

- Kuwa mwenye haki kwa Yesu kulitamkwa na kuimarishwa na Pilato. "Sikuona sababu…" Pilato alitaka kumwachilia huru Yesu hadi Wayahudi walipomweka Yesu juu

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

ya mfalme wake. Sasa Pilato alipaswa kuchagua kati ya wafalme wawili. Je angekuwa Yesu Mfalme wa Wayahudi au Kaisari mfalme wa himaya ya Waroma? Pilato alichagua Kaisari chaguo la watu, mfalme aliyewatawala kama taifa na kuwatesa kama watu. Hakutaka kusikia chochote kuhusu Yesu, ambaye alishuhudia ukweli na kutoa uzima isio na mwisho (Yohana 10:10). Pilato alifanya chaguo baya. Aliweka mfalme mbovu.

**MATUMIZI**:

- Mfalme wako ni nani? Ni nani uliyemkaribisha maishani mwako na kuketi kwenye kiti cha enzi na kutawala moyo na mawazo yako? _____
- Tumia muda kuelezea mfalme wako: _____ _____
- Ni vipi kuhusu mfalme wako kufanya mfalme wako akuvutie? _____ _____

**KUKARIRI**: Pilato alikuwa sahihi aliposema kuwa hakuona kosa lolote kwake. Hakuona msingi wa kuanzia kumuhukumu Yesu. Yesu alikuwa Mwana kamili wa Mungu aliyekuja kama mwana wa mtu kuwa badala yetu, kufa kwaniaba yetu. (1 Yohana 1:7)_____. Kama hujaweka mstari huu kwenye kumbukumbu yako hakikisha kuwa unauweka sasa hivi. Kwa maneno haya machache tunapata uhakika kuwa damu ya Yesu iliyomwangika inatosha kusafisha ndani ya roho zetu. Tunaoshwa safi katika damu ya Mwanakondoo wa Mungu anayeondoa dhambi za ulimwengu (Yohana 1:29).

**SALA**: Bwana Yesu, Ninaona unateswa na kuaibishwa kwasababu ya dhambi zangu. Ninaona ukiwa umekaa karibu na Pilato nasisi sote kwenye umati tukipiga kelele, "Msulubishe! Msilubishe!" Pasipokujali yote ninayoyaona kwa macho yangu ya rohoni, ninaweza tu kukushukuru na kukutukuza. Upendo wako wa milele ni kwaajili yangu na wote wanaopiga kelele kwenye umati. Asante kwa kumwaga damu yako ili niweze kuwa safi kutoka kwenye maovu yangu yote. Dhambi zangu zimeondoka kwasababu yako. Kwa Roho wako niwezeshe kuamini ukweli huu na kunipa pumziko la roho yangu. _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

_____

_____

_____

**Sehemu ya 3**

**UTANGULIZI**: Yesu amekabidhiwa naYuda kwa maaskari katika Gethsemane, kisha kukabidhiwa kwaWakuu wa Makuhani, Pilato, Herode, na kurudishwa kwa Pilato tena. Sasa Pilato amemtoa Yesu kwa kufuata mapenzi ya umati wa watu, mwisho, anakabidhiwa kwa maaskari ili wampeleke aende kusulibishwa. Kifo chake kinakaribia. Anakuja kubebeshwa msalaba wake. Ni lazima atembee kwa miguu barabara inayoelekea Golgotha, Mahali pa Fuvu la Kichwa (Marko 15:22).

**KAZI YA KUFANYA**: Tutazame kimsingi maelezo ya Luka na Yohana kuhusu kusulibisha. Soma Luka 23:26-43 Yohana 19:16b-27. Wengine walifuata. Wengine walibeba misalaba. Wengine walilia na kuomboleza. Wengine walifyonza na kudhiaki. Wengine walimrushia kejeli. Mmoja aliomba. Mmoja alitoa. Mmoja alisamehe. unaposoma, jiangalie katika umati. Usiogope kwenda msalabani sogea karibu ili usikilize, na kusikia maneo ya mwisho ya Yesu. Kumbuka: unahimizwa kusoma kila maelezo ya Injili yanayohusu kusulibisha ambayo pia yanapatikana katika Mathayo 27:32-44 na Marko 15:21-32 kusaidia kumaliza habari.

**ZOEZI** (Kutoka Luka 23):

1. Maaskari walimpeleka Yesu. Kwa vyovyote, alikuwa amechoka kwa mateso na misukosuko aliyofanyiwa na maaskari. Ni nani aliyelazimishwa kubeba msalaba wa Yesu (mstari 26)? _____
   Tunaambiwa nini kuhusu Yeye? _____ Marko 15:21 inatwambia kuwa Simoni alikuwa baba wa _____ na _____. Kwa vyovyote alikuwa kiongozi wa wakristo wa kanisa la kwanza. Simoni alikuwa akitoka Kirene, Libya ya sasa.

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

2. Tunaona Simoni akimfuata Yesu katika mstari wa 26. Ni nani anayefuata katika mstari wa 27? _____

   _____

3. Yesu asingesulibiwa peke yake. Ni aki na nani walioogozana naye (matari wa 32)?

   _____

4. Walifika sehemu inayoitwa _____ (mstri 33).
5. Ni neno gani la kwanza tunalosikia Yesu akisema (mstari 34a)? _____

   _____

6. Na maaskari waliomsulibisha _____ _____ (mstari 34b)
7. Watu wanafanya nini (mstari 35)? _____
8. "…na watawala _____. Walisema, "_____ _____."
9. Vipi kuhusu walinzi? Walifanya nini (mstari 36)? _____ walimpa _____ na kusema, "_____ _____."

   Kumbuka: kibao cha kuthibitisha kosa lake kilivyosomeka (mstari 38)? _____

   _____

10. Mmoja wa waarifu aliyetundiwa pale _____ (mstari 39). Alimtupia dhiaka gani Yesu? _____

    _____

11. Lakini waarifu wengine _____ (mstari 40). Unamsikia akiseme nini kwa washitaki (mstari 40-41)?
    a. Usi _____
    b. Sisi_____
    c. Lakini

       _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

12. Baada ya kusema hayo alimgeukia Yesu na kusema, "_____
_____ (verse 42)."
13. Yesu alijibu, "_____ utakuwa _____ _____ in _____ (mstari 43)."

**Sehemu 4**

**KUTAFAKARI**: Sehemu ya maandiko (Luka 23:26-43) ina mambo ya msingi ya kukumbuka. Hebu tuangalie machache na kuomba Roho wa Mungu atuongoza katika kutambua kwa undani upendo wa Yesu kwajili yetu, ambao ulimfanya ateseke na kufa.

Tunaambiwa kuwa Simoni alimfuata Yesu akiwa amebeba msalaba, ambao kama si upendo wa Baba ingekuwa asulibiwe yeye. Aliubeba msalaba akamfuata Yesu. Yesu aliwaambia nini wanafunzi wake kabla katika huduma yake, alipojaribu kuzungumza nao kuhusu kufa kwake (Mathayo 16:24-25)? _____
_____

- Tunaambiwa kuwa watu walimfuata, wakiwamo "walioomboleza na kumlilia." Wanawake walimtumikia Yesu katika huduma yake yote (Luka 8:2). Iliwaumizaje walipoona ukatili aliokuwa anafanyiwa Yesu, rafiki yao. Kufa kwake kusingehepukika, ndiyo upendo wake mkubwa kwaajili yao, ambao ulimlazimisha kuteseka na kufa.
- Hata mahali pa msalaba wake unabii wake ulitimia. Isaya 53:12 inatwambia nini? Maana ya msalaba wa Yesu kuwekwa katikati ya waalifu wawili? ___
_____
- Luka 4:1-13 anaandika habari za Yesu alipojaribiwa na shetani jangwani. Soma habari hii na onyesha majaribu katika mistari ya 3, 6, na 9. Shetani anatumia maneno haya "ikiwa wewe ni mwana wa Mungu…" kaika majaribu matatu. Kisha kutoweza kumshinda Yesu, Mstari wa 13 unasema kuwa (shetani) _____ _____ _____."  Katika Luka 23 tunaweza kusikia maneno yaleyale yakitumika…
    - Watawala (mstari 35): _____
    - Na maaskari (mstari 37): _____
    - Na mmoja wa waalifu (matari 39): _____

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES

Kwakutumia msalabani shetani alipata "fursa yake" na kisha anamjaribu Yesu akisema, "kama ni wewe yule uliyesema kuwa ndiye, hupaswi kufanya hili. Hakikishia kila mtu kuwa Wewe ni nani kwa kutenda muujiza wa mwisho. Jiokoe. Shuka kutoka msalabani. Tuhakikishie kuwa wewe ni Masihi, Kristo, Aliye teuliwa, Mfalme wa Wayahudi." mmoja msalabani akipata mateso kama hayo anamjaribu, Yesu ni mhanga wa majaribu ya shetani. Tunapata ufahamu gani toka Yohana 12:27? Yesu alikuwa akizungumza na wanafunzi wake kuhusu kitakachotokea. "…nitasema nini? 'Baba, _____'? Hapana, ilikuwa _____."

**KUFUNGA**: Somo hili la kwanza linamalizika ghafla. Yesu amesulibiwa. Amewaombea waliofanya hivi na amemuahidi mwizi aliyesulibiwa upandeni mwake "Leo utakuwa pamoja nami paradiso." Tunafikia hitimisho la sehemu I, kitabu cha 14. Tuko tayari kuanza *Upendo wa Mungu Maisha Yetu – Sehemu ya 11*, kitabu cha15.

Katika Yohana 15:13 tunaambiwa kuwa, "Hakuna mwenye upendo mkuu kama huu, kwa kutoa uhai wake kwaajili ya rafiki zake." Hili ndilo Yesu alilotufanyia, rafiki zake. Habari hiishii na Yesu kutundikwa msalabani. Habari inaisha kwa habari njema ya milele! Unashauriwa kuendelea kwa kuanza *Upendo wa Mungu Maisha Yetu – sehemu ya 11*!

 ©2011 FULLVALUE MINISTRIES